

MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA



Tanzania Food & Drugs Authority

**TAARIFA YA UTENDAJI KAZI  
2016/17**




<b>DHIMA</b>	Kulinda afya ya jamii kwa kuzuia athari zinazoweza kujitokeza kutohana na matumizi ya chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba.
<b>DIRA</b>	Kuwa Mamlaka inayoongoza barani Afrika katika kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba kwa wote.
<b>FALSAFA</b>	Kutoa huduma bora za udhibiti katika kulinda afya ya jamii na mazingira kwa kutumia wafanyakazi wenye ujuzi na ari ya kazi.
<b>MISINGI YA KAZI</b>	<ul style="list-style-type: none"><li>• Kufanya kazi kwa ushirikiano</li><li>• Uaminifu</li><li>• Kuzingatia mahitaji ya wateja</li><li>• Ubora</li><li>• Uwajibikaji</li></ul>

## **BARUA YA KUWASILISHA**



**Mhe.Ummy A. Mwalimu (Mb),**  
Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii,  
Jinsia, Wazee na Watoto,  
Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Kitivo cha Sanaa ya Sayansi ya  
Maendeleo ya Jamii, Jengo Na 11  
S.L.P 743,  
404780 Dodoma



**Dkt. Mpoki M. Ulisubisywa,**  
Katibu Mkuu (Afya),  
Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii,  
Jinsia, Wazee na Watoto,  
Kitivo cha Sanaa ya Sayansi ya  
Maendeleo ya Jamii, Jengo Na. 11  
S.L.P 743,  
404780 Dodoma

Mhe. Waziri,

Ninayo heshima kubwa kuwasilisha kwako Taarifa ya Utendaji Kazi ya Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) kwa kipindi cha mwaka 2016/17. Taarifa hii imeeleza utekelezaji wa shughuli za TFDA katika kutimiza lengo lake kuu la kulinda afya ya jamii kwa kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi.

Ninawasilisha.

A handwritten signature in black ink, appearing to read "Mpoki".

**Dkt. Mpoki M. Ulisubisywa**  
**Katibu Mkuu (Afya)**

## **MAELEZO YA MWENYEKITI WA BODI YA USHAURI (MAB)**

Huu ni mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa miaka mitano (5) wa TFDA (2012/13 - 2016/17) ambao umelenga kuimarisha utekelezaji wa jukumu la msingi la kulinda afya ya jamii kwa kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi.

Katika kipindi hiki cha 2016/17, Mamlaka imeendelea kuboresha utoaji huduma kwa wateja kwa kutumia mifumo ya kieletroniki kutekeleza mifumo bora ya kiutendaji (Quality Management System) kwa kiwango cha kimataifa cha ISO 9001:2015. Aidha, Mkataba wa Huduma kwa Wateja ulifanyiwa mapitio kwa kuboresha viwango vya utoaji huduma ili kukidhi mahitaji na matarajio ya wateja.

TFDA pia imeendelea kuwekeza katika ununuzi wa vifaa vya maabara vya kisasa na kukamilisha ujenzi wa maabara ya Kanda ya Ziwa, Mwanza pamoja na kuwajengea uwezo wataalamu wa maabara. Aidha, Maabara ya Chakula na Maikrobiolojia zimefanikiwa kushikilia cheti cha ithibati (accreditation) kwa kiwango cha Kimataifa cha ISO/IEC 17025:2015 baada ya kukaguliwa na taasisi za ithibati za SADCAS/SANAS. Hii inafanya matokeo ya chunguzi zinazofanywa na maabara kutambuliwa kimataifa.

Vilevile, vitabu vya hesabu na rasilimali za Mamlaka kwa kipindi kinachoishia Juni 2016, zilikaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na TFDA kupata hati safi.

Naipongeza Menejimenti pamoja na wafanyakazi wote wa TFDA kwa kufanya kazi kwa weledi na kujituma katika kufikia matarajio ya wateja. Vilevile, natoa shukrani kwa wadau wote wa Mamlaka ikiwa ni pamoja na jamii kwa ujumla kwa ushirikiano wao katika kusaidia TFDA kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Nichukue fursa hii pia kutoa wito kwa wadau wote wa TFDA kutekeleza wajibu wao ipasavyo kwa kutoa taarifa na kushirikiana na Mamlaka katika kuhakikisha kuwa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi viliyyopo katika soko vinakidhi vigezo vya ubora na usalama.

Bodi ya Ushauri ya Wizara (MAB) chini ya uenyekiti wangu itaendelea kutoa maelekezo kwa Menejimenti ya TFDA sanjari na ushauri kwa Wizara katika kuhakikisha kuwa afya ya jamii inalindwa dhidi ya madhara yanayoweza kujitokeza kutohana na kutumia chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi.



**Balozi Dkt. Ben Moses**

**MWENYEKITI WA BODI YA USHAURI**

## **MAELEZO YA MKURUGENZI MKUU**

Taarifa hii ya utendaji kazi kwa mwaka 2016/2017 inaanisha hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezeji wa kazi na majukumu ya TFDA, mafanikio yaliyopatikana katika kipindi tajwa pamoja na maeneo yanayohitaji kupewa kipaumbele kwa mwaka 2017/18. Aidha, changamoto mbalimbali zilizoikabili Mamlaka na mbinu zilizotumika na zinazoendelea kutumika katika kuzikabili zimeainishwa. Utekelezaji wa malengo mkakati sita (6) ya Mpango Mkakati wa miaka (5) ya TFDA (2012/13 – 2016/17) ni mambo ya msingi yaliyozingatiwa katika Taarifa hii.

Katika utekelezaji wa lengo la kuimarisha udhibiti wa ubora, usalama na ufanisi wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba; Mamlaka ilikuwa na jumla ya maombi ya usajili wa bidhaa 10,075 ambapo 651 ni baki ya maombi ya mwaka 2015/2016. Maombi 9,442 sawa na 93.7% yalitathminiwa na kati yake maombi 4,609 sawa na 49% yaliidhinishwa. Maombi yaliyofanyiwa tathmini ni ongezeko la maombi 863 (10%) ikilinganishwa na maombi 8,579 yaliyotathminiwa mwaka 2015/2016. Hii ni kutokana na kukua kwa matumizi ya mfumo wa kielektroniki katika utoaji huduma za TFDA ambaa umefupisha muda wa watumishi kushughulikia maombi mbalimbali.

Katika kipindi husika, kulikuwa pia na mafanikio katika usajili wa maeneo na utoaji vibali vyta biashara ya chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba ambapo jumla ya maombi 9,706 yalikuwepo ikiwa ni pamoja na maombi 198 yaliyobaki mwaka 2015/2016. Maombi 9,605 sawa na 99% yalitathminiwa ambapo maombi 9,000 sawa (94%) yaliidhinishwa. Idadi hii inajumuisha viwanda vipyta 617 vyta chakula vilivyosajiliwa kupitia ofisi za Kanda. Maombi ya usajili wa maeneo ya kuendesha biashara yaliyokuwepo ni ongezeko la maombi 2,194 sawa na 29% ikilinganishwa na maombi 7,512 yaliyokuwepo mwaka 2015/16. Ongezeko hili linatokana na juhudhi zilizofanywa katika kazi za udhibiti hususan ukaguzi wa mara kwa mara wa bidhaa na vibali vyta maeneo ya biashara pamoja na elimu kwa wadau ili kuhamasisha utii wa sheria kwa hiari.

Kupitia kazi ya ukaguzi na ufuatiliaji wa usalama na ubora wa bidhaa, maeneo 17,314 yanayojihusisha na biashara ya chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba yalikaguliwa. Maeneo haya yamejumuhisha viwanda, maghala, magari, machinjio, na maeneo ya kuuzia bidhaa zinazodhibitiwa na TFDA. Idadi hii ni ongezeko la maeneo 10,481 (153%) ikilinganishwa na maeneo 6,833 yaliyokaguliwa mwaka 2015/16.


Vilevile, maombi 15,738 ya vibali vyta kuingiza na kusafirisha vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba ndani na nje ya nchi yalipokelewa ambapo vibali 15,571 sawa na 99% vilitolewa. Vilevile, katika mwaka 2016/2017, jumla ya sampuli 4,914 sawa na 94.4% kati ya sampuli 5,203 za bidhaa zilizokuwepo zilichunguzwa ambapo sampuli 4,722 (96.1%) zilifafulu. Matokeo haya ni kiashiria cha uwepo wa bidhaa nyingi zenyenye ubora na usalama unaokubalika katika soko la Tanzania.

Kwa upande wa usimamizi wa rasilimali, Mamlaka ilikusanya jumla ya TZS 43.7 bilioni kutoka vyanzo mbalimbali vilivyoainishwa katika mpango kazi na bajeti ya mwaka 2016/2017 ambapo kati ya kiasi hiki, TZS 34.4 bilioni sawa na 79% zilitokana na makusanyo ya ada na tozo, TZS 3.3 bilioni ni kutoka Serikali Kuu na TZS 350 milioni zilipokelewa kutoka Washirika wa Maendeleo.

Mamlaka pia ilitumia kiasi cha TZS 37.2 bilioni kwa ajili ya kutekeleza kazi zilizopangwa, kulipia huduma na mipango ya maendeleo hususan ukamilishwaji wa ujenzi wa maabara na ofisi ya TFDA Kanda ya Ziwa, Mwanza.

Pamoja na mafanikio haya, kuna baadhi ya maeneo ambayo yanahitaji kupewa kupaumbele kwa mwaka 2017/18, ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya TFDA. Maeneo hayo ni pamoja na

kutoa elimu zaidi juu ya namna ya kujikinga na madhara yanayosababishwa na sumukuvu, kuongeza kasi ya kufanya tathmini, usajili na ukaguzi, kuwatambua na kuwajengea uwezo wazalishaji wadogo wa bidhaa zinazodhibitiwa na TFDA na kuimarisha mifumo ya kielektroniki katika utoaji huduma.Vile vile, Mamlaka inatarajia kufanya upanuzi wa maabara ya uchunguzi wa dawa makao makuu kukamilisha ununuzi wa vifaa vya maabara ya kanda ya ziwa, Mwanza na kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi ili kuongeza weledi, tija na ufanisi katika kazi.



**Hiiti B. Sillo**

**MKURUGENZI MKUU**

## 1. UTANGULIZI

Mwaka 2016/17 ni wa mwisho wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa miaka mitano (5) wa TFDA wa 2012/13 - 2016/17. Mpango Mkakati huo umelenga kutekeleza jukumu la kulinda afya ya jamii kwa kudhibiti ubora na usalama wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba pamoja na udhibiti wa vitendanishi.

Kazi zilizotekelawa kwa mwaka 2016/17 zimezingata malengo mahususi sita (6) ya Mpango Mkakati huo kama ilivyoainishwa hapa chini:-

- (a) Kuimarisha udhibiti wa ubora, usalama na ufanisi wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba;
- (b) Kuimarisha utoaji elimu na shughuli za kutangaza huduma za Mamlaka;
- (c) Kuimarisha usimamizi wa rasilimali;
- (d) Kutoa huduma kwa waathirika na kupunguza maambukizi ya Virusi vya UKIMWI;
- (e) Kuimarisha na kutekeleza kwa ufanisi Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa; na
- (f) Kuboresha masuala ya Jinsia na Mazingira.

## 2.0 KUIMARISHA UBORA, USALAMA NA UFANISI WA CHAKULA, DAWA, VIPODOZI NA VIFAA TIBA

### 2.1 Tathmini na usajili wa vyakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na matangazo

Mamlaka ilikuwa na baki ya maombi ya tathmini ya bidhaa 651 kwa mwaka 2015/16 na kupokea maombi 9,424; hivyo kufanya jumla ya maombi yote ya usajili pamoja na matangazo ya bidhaa kuwa 10,075. Maombi yaliyokuwepo kwa ajili ya tathmini ni ongezeko la maombi 1,607 (17%) ikilinganishwa na maombi 8,579 yaliyokuwepo mwaka 2015/16.

Kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa Mamlaka kwa mwaka 2016/17, lengo ilikuwa ni kutathmini 90% ya maombi ya chakula, 75% dawa, 80% vipodozi na 95% vifaa tiba ifikapo Juni, 2017. Maombi 9,442 sawa na 93.7% yalifanyiwa tathmini ambapo maombi 4,607 sawa na 49% yaliidhinishwa. Maombi 225 yalikataliwa na mengine 2,796 yalikuwa na haoja mbalimbali za kujibu kabla ya maamuzi ya kuyaidhinisha au kukataliwa .Mchanganuo wa maombi ya usajili wa bidhaa umeainishwa katika Jedwali 1 (a).

*Jedwali Na.1 (a): Mchanganuo wa Maombi ya sajili wa vyakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba, matangazo na majaribio ya dawa*

Na.	Aina ya bidhaa	Maeleo	Baki 2015/16	Pokelewa	Jumla	Tathminiwa	Baki	Idhinishwa	Kataliwa	Hoja
1	Chakula	Mapya	232	2045	2277	2169	108	1452	165	552
		Huishwa	0	94	94	93	1	59	2	32
		Lebo	12	152	164	163	1	55	0	108
		Mabadiliko	0	11	11	11	0	11	0	0
		Majibu ya Hoja	0	628	628	617	11	NA	NA	NA
	<b>Jumla ndogo</b>		<b>244</b>	<b>2930</b>	<b>3174</b>	<b>3053</b>	<b>121</b>	<b>1577</b>	<b>167</b>	<b>692</b>

Na.

## Aina ya bidhaa


				Maelezo	Baki 2015/16	Pokelewa	Jumla	Tathminiwa	Baki	Idhnishwa	Kataliwa	Hoja
2	Dawa	Binadamu	Mapya	68	556	624	583	41	277	16	290	
			Huishwa	14	450	464	436	28	307	0	129	
3	Majaribio ya dawa	Antiseptics na Disinfectants	Mabadiliko	8	679	687	656	31	579	0	77	
			Majibu ya Hoja	23	901	924	885	39	NA	NA	NA	
			<b>Jumla ndogo</b>	<b>113</b>	<b>2586</b>	<b>2699</b>	<b>2560</b>	<b>139</b>	<b>1163</b>	<b>16</b>	<b>496</b>	
			Mapya	8	43	51	48	3	23	4	21	
			Huishwa	16	42	58	54	4	47	0	7	
3	Mitishamba	Mifugo	Mabadiliko	0	10	10	10	0	6	0	4	
			Majibu ya Hoja	4	100	104	102	2	NA	NA	NA	
			<b>Jumla ndogo</b>	<b>28</b>	<b>195</b>	<b>223</b>	<b>214</b>	<b>9</b>	<b>76</b>	<b>4</b>	<b>32</b>	
			Mapya	1	9	10	10	0	3	0	7	
			Huishwa	0	0	0	0	0	0	0	0	
3	Antiseptics na Disinfectants	Mitishamba	Mabadiliko	0	0	0	0	0	0	0	0	
			Majibu ya Hoja	0	0	0	0	0	0	0	NA	
			<b>Jumla ndogo</b>	<b>1</b>	<b>9</b>	<b>10</b>	<b>10</b>	<b>0</b>	<b>3</b>	<b>0</b>	<b>7</b>	
			Mapya	22	90	112	108	4	3	1	104	
			Huishwa	0	0	0	0	0	0	0	0	
3	Majaribio ya dawa	Antiseptics na Disinfectants	Mabadiliko	0	0	0	0	0	0	0	0	
			Majibu ya Hoja	0	24	24	24	0	NA	NA	NA	
			<b>Jumla ndogo</b>	<b>22</b>	<b>114</b>	<b>136</b>	<b>132</b>	<b>4</b>	<b>3</b>	<b>1</b>	<b>104</b>	
			Mapya	0	16	16	16	0	10	0	6	
			Mabadiliko	0	22	22	22	0	22	0	0	
3	Mitishamba	Antiseptics na Disinfectants	Majibu ya Hoja	4	15	19	16	3	NA	NA	NA	
			<b>Jumla ndogo</b>	<b>4</b>	<b>53</b>	<b>57</b>	<b>54</b>	<b>3</b>	<b>32</b>	<b>0</b>	<b>6</b>	

Na.

		Aina ya bidhaa		Maelezo	Baki 2015/16	Pokelewa	Jumla	Tathminiwa	Baki	Idhinishwa	Kataliwa	Hoja
4	Vipodozi	Mapya	199	876	1075	971	104	1033	29	0		
		Huishwa	14	319	333	330	3	340	8	0		
		Mabadiliko	3	41	44	38	6	38	0	0		
		Majibu ya Hoja	0	71	71	71	0	NA	NA	NA		
		<b>Jumla ndogo</b>	<b>216</b>	<b>1307</b>	<b>1523</b>	<b>1410</b>	<b>113</b>	<b>1411</b>	<b>37</b>	<b>0</b>		
5	Vifaa tiba	Mapya	13	172	185	179	6	70	0	109		
		Huishwa	0	55	55	30	25	0	0	30		
		Mabadiliko	0	38	38	28	10	6	0	22		
		Majibu ya Hoja	2	269	271	205	66	NA	NA	NA		
		<b>Jumla ndogo</b>	<b>15</b>	<b>534</b>	<b>549</b>	<b>442</b>	<b>107</b>	<b>76</b>	<b>0</b>	<b>161</b>		
6	Vitendanishi	Mapya	0	1447	1447	1321	126	75	0	1246		
		Jumla ndogo	0	1447	1447	1321	126	75	0	1246		
7	Matangazo	Chakula	Mapya	0	11	11	11	0	4	0	7	
		Dawa	Mapya	4	152	156	152	4	107	0	45	
			Majibu ya Hoja	0	3	3	3	0	NA	NA	NA	
	Vipodozi	Mapya	4	83	87	80	7	80	0	0		
		<b>Jumla ndogo</b>	<b>8</b>	<b>249</b>	<b>257</b>	<b>246</b>	<b>11</b>	<b>191</b>	<b>0</b>	<b>52</b>		
	<b>Jumla Kuu</b>		<b>651</b>	<b>9424</b>	<b>10075</b>	<b>9442</b>	<b>633</b>	<b>4904</b>	<b>225</b>	<b>2744</b>		

NA = Majibu ya hoja hayaidhinishwi wala kukataliwa.

### *Mchoro Na. 1: Maombi yaliyokuwepo na Kutathminiwa*



### *Jedwali Na. 1 (b): Utekelezaji wa lengo la usajili wa bidhaa kwa mwaka 2016/17*

Na.	Maelezo	Bidhaa						
		Chakula	Dawa		Vipodozi	Vifaa tiba	Majaribio ya Dawa	
			Binadamu	Mifugo				
1	Idadi ya maombi kwa ajili ya tathmini (A)	3,174	2,699	223	1,523	549	57	
2	Lengo la Mpango Mkakati wa miaka mitano (5)	90%	75%	75%	80%	95%	95%	
3	Idadi ya maombi yanayopaswa kutathminiwa (B)	2,857	2,024	167	1,218	522	54	
4	Idadi ya maombi yaliyotathminiwa (C)	3,053	2,560	214	1,410	442	54	
5	% ya maombi yaliyotathminiwa (C/A*100)	96%	95%	96%	93%	81%	95%	
6	% ya utekelezaji wa lengo mkakati (C/B*100)	107%	126%	128%	116%	85%	100%	

Kwa mujibu wa Jedwali Na. 1 (a) na 1(b) hapo juu, malengo yaliyopangwa kwa mwaka 2016/17 ya usajili wa chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na majaribio ya dawa yamefikiwa na kuvukwa isipokuwa kwa tathmini ya vifaa tiba. Mpango maalum wa kuwashirikisha watathmini wa ndani na nje ya TFDA utatumika kwa mwaka 2017/18 katika usajili wa vifaa tiba.

**Jedwali Na. 1(c): Mchanganuo wa maombi mapya ya bidhaa ambayo hayajafanyiwa tathmini kulingana na umri wa kupokea (Age analysis)**

Na.	Aina ya bidhaa	Mkataba wa huduma kwa wateja (siku)	≤45	46-60	61-130	131-200	201-240	> 240	Jumla
1.	Chakula	vyakula vyenye hatari ndogo	45	95	0	0	0	0	95
		Vyakula vyenye hatari kubwa	60	13	0	0	0	0	13
2.	Dawa za binadamu	240	41	0	0	0	0	0	41
3.	Dawa za mifugo	240	3	0	0	0	0	0	3
4.	Dawa za Mitishamba	200	0	0	0	0	0	0	0
5.	Bidhaa nyongeza (Antiseptics na Disinfectants)	200	4	0	0	0	0	0	4
6.	Vipodozi	50	104	0	0	0	0	0	104
7.	Vifaa tiba	200	6	0	0	0	0	0	6
<b>JUMLA</b>			<b>266</b>	<b>0</b>	<b>0</b>	<b>0</b>	<b>0</b>	<b>0</b>	<b>266</b>

Kwa mujibu wa Jedwali Na. 1.(C) hapo juu, maombi mapya ambayo hayajafanyiwa tathmini yapo ndani ya muda ulioainishwa katika Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa mwaka 2016.

## 2.2. Usajili wa maeneo na utoaji wa vibali vya biashara ya vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba

Katika kipindi hiki cha 2016/17, Mamlaka ilikuwa na maombi 9,706 ya usajili wa maeneo ya biashara za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba. Maombi haya yanajumuisha mapya, kuhuisha na baki ya maombi 198 ya mwaka 2015/16. Maombi yaliyokuwepo mwaka huu ni ongezeko la maombi 2,190 sawa na 29% ikilinganishwa na maombi 7,512 ya usajili wa maeneo ya kuendesha biashara za bidhaa zinazodhitibwa na Mamlaka kwa mwaka 2015/16.

Maombi 9,605 sawa na 99% yalifanyiwa tathmini ikilinganishwa na lengo la kutathmini 100% ya maombi yote yanayopokelewa kwa mwaka. Jumla ya maombi 9,000 sawa na 94% ya maombi yaliyofanyiwa tathmini, yalikidhi vigezo na kuidhinishwa. Idadi hii inajumuisha viwanda vipyta 617 vya chakula vilivyosajiliwa na TFDA kuitia ofisi za Kanda. Mchanganuo wa maombi hayo ni kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 2(a) na 2(b).

*Jedwali Na. 2(a): Maombi ya Usajili wa Maeneo na Utoaji wa Vibali vyatashara ya vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba*

Aina ya jengo		Baki kutoka 2015/16	Yaliyopokelewa		Jumla	Yaliyotathminiwaa	Yaliyyosajiliwa	Asilimia katika kukidhi vigezo
			Mapya	Huishaa				
Chakula	Viwanda	43	617	595	1255	1209	1060	88%
	Maghala	30	355	309	694	694	576	83
	Hotelii	0	116	159	275	275	266	97
	Kuuzia chakula- jumla	0	94	61	155	155	149	96
	Kuuzia chakula-reja reja	32	1633	1452	3117	3071	2972	97
	Machinjio	0	7	6	13	11	8	73
	Magari ya kubebaa chakula	0	225	430	655	655	650	99
<b>Jumla ndogo</b>		<b>105</b>	<b>3047</b>	<b>3012</b>	<b>6164</b>	<b>6070</b>	<b>5681</b>	<b>94</b>
Dawa	Viwanda vya ndani	0	1	4	5	5	4	80
	Maghala	0	8	32	40	40	39	98
	Duka la dawa-Binadamu	7	22	79	108	108	101	94
	Duka la dawa-Mifugo	24	222	121	367	367	317	86
	Magari	0	8	3	11	11	4	36
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>31</b>	<b>261</b>	<b>239</b>	<b>531</b>	<b>531</b>	<b>465</b>	<b>88</b>
Vipodozi	Watengenezaji	23	17	8	48	47	22	47
	Wauzaji wa Jumla	6	87	136	229	226	217	96
	Wauzaji Rejareja	5	1188	1252	2445	2442	2363	97
	Maghala	5	72	40	117	117	107	91
	Magari ya kubebaa vipodozi	0	3	7	10	10	10	100
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>39</b>	<b>1367</b>	<b>1443</b>	<b>2849</b>	<b>2842</b>	<b>2719</b>	<b>96</b>
Vifaa tiba	Wauzaji wa jumla	23	85	51	159	159	132	83
	Maghala	0	3	0	3	3	3	100
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>23</b>	<b>88</b>	<b>51</b>	<b>162</b>	<b>162</b>	<b>135</b>	<b>83</b>
<b>Jumla Kuu</b>		<b>198</b>	<b>4763</b>	<b>4745</b>	<b>9706</b>	<b>9605</b>	<b>9000</b>	<b>94%</b>

Idadi ya maombi yaliyofanyiwa tathmini kwa mwaka 2016/17 ni ongezeko la maombi 2,333 (32%) ikilinganishwa na maombi 7,272 yaliyofanyiwa tathmini mwaka 2015/16. Vilevile, idadi ya maeneo yaliyokidhi vigezo na kusajiliwa ni ongezeko la maombi 3,394 (61%) ikilinganishwa na maombi 5,606 yaliyosajiliwa mwaka 2015/16.

Ongezeko hili la idadi ya maombi yaliyotathminiwa na kuongezeka kwa idadi ya maeneo yaliyokidhi vigezo inatokana na juhudzi zilizofanywa katika kazi za udhibiti ikiwemo mafunzo ya wadau hususan wajasiriamali kuhusu kutii sheria kwa hiari na kuchangia katika kuhakikisha kuwa afya ya walaji inalindwa.

***Jedwali Na. 2(b): Mchanganuo wa makundi ya viwanda vya chakula viliviyosajiliwa kwa kila Kanda kwa kipindi cha mwaka 2016/17***

Na.	Ofisi ya Kanda	Viwanda vidogo (Small scale food)	Viwanda vya kati (Medium scale)	Viwanda vikubwa (Large scale)	Jumla
1	Mashariki	176	21	0	197
2	Kaskazini	46	19	0	65
3	Ziwa	96	42	27	165
4	Kusini	16	17	1	34
5	Magharibi	26	6	0	32
6	Nyanda za Juu Kusini	12	13	4	29
7	Kati	75	12	8	95
<b>JUMLA</b>		<b>447</b>	<b>130</b>	<b>40</b>	<b>617</b>

**2.3 Ukaguzi na ufuatiliaji wa usalama na ubora wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba**

Katika kipindi hiki cha 2016/17, Mamlaka ilifanya ukaguzi na ufuatiliaji kwenye maeneo yanayojihusisha na biashara ya chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba ambapo jumla ya maeneo 17,314 yalikaguliwa. Maeneo hayo ni pamoja na viwanda, maghala, machinjio, magari na maeneo ya kuuzia bidhaa zinazodhibitiwa na TFDA.

Idadi ya maeneo yaliyokaguliwa katika kipindi hiki ni zaidi ya maeneo 10,481 (153%) ikilinganishwa na maeneo 6,833 yaliyokaguliwa mwaka 2015/16. Ongezeko hili limechangiwa na kuongezeka kwa mwamko wa kuanzisha viwanda na kurasimisha biashara mionganoni mwa wafanyabiashara sanjari na ongezeko la idadi ya wakaguzi wa Mamlaka. Mchanganuo wa maeneo yaliyokaguliwa umeainishwa kwenye Jedwali na. 3.

*Jedwali Na. 3: Maeneo yaliyokaguliwa katika kipindi cha mwaka 2016/17*

Na.	Aina ya biashara	Idadi ya maeneo yaliyokaguliwa		Idadi ya maeneo yaliyokidhi vigezo	
		Idadi	idadi	%	
1	Chakula	Viwanda (Ndani ya nchi)	2517	1447	57%
		Sehemu za kuuzia	5762	3937	68%
		Maghala	591	421	71%
		Hoteli	45	41	91%
		Magari	158	81	51%
		Machinjio	239	100	42%
		Viwanda vyatya nje	8	7	88%
	<b>Jumla ndogo</b>		<b>9320</b>	<b>6034</b>	<b>65%</b>
2	Dawa	Famasi na DLDM - binadamu	2701	1944	72%
		Famasi na DLDM- mifugo	741	526	71%
		Viwanda vyatya dawa (Ndani ya nchi)	11	4	36%
		Viwanda vyatya dawa (Nje ya nchi)	119	65	55%
		Maeneo ya kutolea Huduma ya Afya			
		(1) Vituo vyatya Afya vyatya Serikali	174	172	99%
		(2) Vituo vyatya Afya vyatya Binafsi	15	15	100%
		(3) Vituo vyatya Afya vyatya Mashirika ya Kidini (FBO)	6	6	100%
		(4) Hospitali	180	180	100%
		(5) Zahanati	165	165	100%
		(6) Maghala	42	30	71%
		(7) Magari	5	5	100%
		<b>Jumla ndogo</b>	<b>4159</b>	<b>3112</b>	<b>75%</b>
3	Vipodozi	Maduka jumla	153	131	86%
		Maduka Rejareja	3398	2864	84%
		Maghala	60	56	93%
		Viwanda	36	11	31%
		Magari	1	1	100%
		<b>Jumla ndogo</b>	<b>3648</b>	<b>3063</b>	<b>84%</b>
4	Vifaa Tiba	Wauzaji wa Jumla	162	136	84%
		Wauzaji wa Rejareja	5	5	100%
		Viwanda (nje ya nchi)	10	9	90%
		Viwanda (ndani ya nchi)	2	0	0%
		Maghala	8	7	88%
	<b>Jumla ndogo</b>		<b>187</b>	<b>157</b>	<b>84%</b>
	<b>Jumla kuu</b>		<b>17,314</b>	<b>12,366</b>	<b>71%</b>

Kwa mujibu wa jedwali Na.3 hapo juu, wastani wa 71% ya maeneo yaliyokaguliwa yalikidhi matakwa ya sheria ikilinganishwa na wastani wa 82% kwa mwaka 2015/16. Kiwango cha kukidhi matakwa ya sheria kimeshuka kwa 1% hasa katika maeneo ya viwanda vya ndani vya vifaa tiba, machinjio, viwanda vya vipodozi na viwanda vya ndani vya chakula.

Kwa mantiki hiyo, jitihada kubwa zinahitaji katika kuimarisha ukaguzi wa maeneo hayo ikiwa ni pamoja na kutoa elimu juu ya umuhimu wa kukidhi matakwa ya sheria na mafunzo kwa wasindikaji wa viwanda vidogo (SMEs) vya chakula na vipodozi. Aidha, machinjio yanatakiwa kuboreshwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wakuu wa Mikoa, Bodi ya nyama Tanzania pamoja na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi katika kuandaa mikakati madhubuti kwa ajili hiyo. Hii ni kufuatia makubaliano ya kikao cha pamoja baina ya taasisi hizi kilichofanyika Morogoro mwezi Januari, 2017.

#### **2.4 Udhibiti wa uingizaji na usafirishaji wa bidhaa ndani na nje ya nchi.**

Mamlaka ilipokea jumla ya maombi 15,738 ya kuingiza na kusafirisha bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba nje ya nchi. Kati ya maombi hayo, 15,571 sawa na 99% ya maombi yote yaliyopokelewa yaliidhinishwa kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali Na. 4.

#### ***Jedwali 4: Mchanganuo wa maombi ya vibali vya kuingiza na kusafirisha bidhaa ndani na nje ya nchi na vibali vilivyokaguliwa katika vituo vya forodha***

Na.	Aina ya bidhaa	Yaliyopokelewa		Vibali vilivyotolewa		Vibali vilivyokaguliwa katika vituo vya forodha	
		Kuingia	Kutoka	Kuingia	Kutoka	Kuingia	Kutoka
1	Dawa	3048	70	3044	70	536	4
2	Vipodozi	1379	752	1301	729	256	273
3	Vifaa tiba	2094	10	2073	10	82	1
4	Chakula	6629	1756	6600	1744	2751	1370
<b>Jumla</b>		<b>13,150</b>	<b>2,588</b>	<b>13,018</b>	<b>2,553</b>	<b>3,625</b>	<b>1,648</b>

Kwa mujibu wa Jedwali Na. 4 hapo juu, upo umuhimu wa kuwa na mfumo wa taarifa wa kielectroniki (IMIS) katika vituo vya forodha kwa ajili ya kufuatilia na kutunza kumbukumbu za vibali vilivyokaguliwa katika vituo hivyo.

#### **2.5 Uchunguzi wa Sampuli katika Maabara ya Mamlaka**

Mamlaka katika mwaka 2016/17 ilipokea sampuli 5,183 na kufanya jumla ya sampuli zilizokuwepo kuwa 5,329 ikiwa ni pamoja na baki ya sampuli 146 za mwaka 2015/16. Kwa mujibu wa Mpango Mkakati, Mamlaka ililenga kuchunguza 90% ya sampuli zilizopo. Kati ya sampuli zilizokuwepo, 5,040 zilichunguzwa ikiwa ni 94.6% ya sampuli zilizopokelewa. Sampuli 4,846 sawa na 96.1 % zilifaulu. Mchanganuo wa uchunguzi wa sampuli kwenye maabara umeainishwa kwenye Jedwali Na.5 hapa chini.

*Jedwali Na. 5: Mchanganuo wa uchunguzi wa sampuli za bidhaa kwa 2016/17*

Bidhaa	Chanzo Cha Sampuli	Baki ya Mwaka 2015/16 (A)	Mpya (B)	Jumla (C) = A + B	Chunguzwa (D)	Faulu (E)	Zisizokidhi (F)	% Faulu
Dawa	Ukaguzi Dawa za Binadamu	6	31	37	36	33	3	91.6
	Pharmacovigilance	5	10	15	15	13	2	86.6
	Ufuatiliaji wa Dawa Binadamu (PMS)	11	359	370	360	344	16	95.5
	Ufuatiliaji wa Dawa Mifugo (PMS)	0	130	130	130	127	3	98
	Uchunguzi wa awali (TFDA - HQ)	49	883	932	799	798	1	99.8
	Uchunguzi wa awali "QA centres"	0	612	612	612	612	0	100
	Wateja wa Nje – Binadamu	0	54	54	42	40	2	95.2
	Malighafi	0	19	19	19	19	0	100
<b>Jumla Ndodo</b>		<b>71</b>	<b>2,098</b>	<b>2,169</b>	<b>2,013</b>	<b>1,986</b>	<b>27</b>	<b>98.7</b>
Vipodozi	Ukaguzi	4	5	9	9	7	2	77.7
	Uchunguzi wa awali	0	4	4	4	4	0	100
	Usajili	0	17	17	17	16	1	94.1
	Ufuatiliaji wa vipodozi (PMS)	4	0	4	4	4	0	100
<b>Jumla Ndodo</b>		<b>8</b>	<b>26</b>	<b>34</b>	<b>34</b>	<b>31</b>	<b>3</b>	<b>91.2</b>
Chakula	Ukaguzi	22	858	880	790	782	8	98.9
	Usajili	15	476	491	470	467	3	99.3
	Wateja wa nje	0	165	165	165	161	4	97.5
	Ufuatiliaji wa bidhaa sokoni	0	921	921	899	756	143	84.1
	Sampuli za utafiti	30	581	611	611	611	0	100
<b>Jumla ndogo</b>		<b>67</b>	<b>3,001</b>	<b>3,068</b>	<b>2,935</b>	<b>2,777</b>	<b>158</b>	<b>94.6</b>
Vifaa Tiba	Ufuatiliaji (PMS)	0	58	58	58	52	6	89.6
<b>Jumla Ndodo</b>		<b>0</b>	<b>58</b>	<b>58</b>	<b>58</b>	<b>52</b>	<b>6</b>	<b>89.6</b>
<b>JUMLA KUU</b>		<b>146</b>	<b>5,183</b>	<b>5,329</b>	<b>5,040</b>	<b>4,846</b>	<b>194</b>	<b>96.1</b>



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mhe. Ummy A. Mwalimu (Mb) akiwa katika ziara ya kikazi kwenye maabara ya TFDA

## 2.6 Utengenezaji na ugezi wa vifaa vyta maabara

Matengenezo ya vifaa vyta maabara (preventive maintenance) yalifanyika kama ilivyopangwa kwa kila robo mwaka ili kuhakikisha mashine husika zinafanya kazi kwa ufanisi. Katika kipindi hiki, mashine 117 zilifanyiwa matengezo ya kawaida ambapo aina 20 za vipuri vilinunuliwa na kufungwa. Aidha, ugezi (calibration) wa vifaa 114 ulifanywa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na vingine nane (8) vilifanyiwa na kampuni ya Archemedes ya nchini Afrika ya Kusini.

## 2.7 Upimaji wa umahiri katika uchunguzi wa sampuli (Proficiency Testing Scheme)

Mamlaka ilishiriki katika uchunguzi wa sampuli mbalimbali za kujipima umahiri ambapo jumla ya vigezo vyta umahiri 96 vilifanyiwa uchunguzi (22 chakula, 15 dawa na 59 mikrobiolojia). Majibu ya vigezo 85 yalipokelewa ambapo Mamlaka ilifanya vizuri katika vigezo 74. Majibu kuhusu vigezo 11 hayakuridhisha (1 dawa, 4 mikrobiologia na 6 chakula) hivyo Mamlaka kufanya tathmini kwenye taratibu sanifu ya utendaji kazi (SOP) kubaini chanzo cha tatizo ambapo hatua stahiki za kurekebisha hali hiyo isijitokeze tena zilichukuliwa.

## 2.8 Ufuatiliaji wa Madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa

### 2.8.1 Utekelezaji wa mpango wa ufuatiliaji wa madhara yatokanayo na chakula

Mamlaka ilipokea taarifa za madhara yaliyohusishwa na matumizi ya chakula ambapo jumla ya watu 41,624 waliripotiwa kuugua katika mikoa ya Dodoma, Rukwa, Manyara, Njombe, Katavi, Lindi, Ruvuma na Singida. Ugonjwa wa kuhara uliongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa ambayo ni 35,012 (84.1%). Hata hivyo, taarifa nyingi za magonjwa hayo hazikuweza kuthibitishwa ingawa zilihuushwa na ulaji wa chakula kisicho salama. Magonjwa mengine yatokanayo na chakula kisicho salama yaliyoripotiwa ni homa ya matumbo 3,546 (8.5%) na kuhara damu 3,057 (7.3%).



Mtaalam wa TFDA akitoa mafunzo kuhusiana na magonjwa yatokanayo na matumizi ya chakula kwa watendaji wa Halmashauri mbalimbali wanaoshirikiana na TFDA katika udhibiti wa usalama wa chakula nchini.

Kutokana na taarifa hii, kipaumbele kimewekwa katika kutoa elimu juu ya kanuni bora za usafi ili kupunguza madhara yatokanayo na uchafuzi wa vimelea vya maradhi katika chakula.

Vilevile, mpango wa ufuatiliaji wa madhara yatokanayo na chakula ulisambazwa katika mikoa saba (7) ambayo ni Lindi, Songwe, Tanga, Ruvuma, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam ambapo jumla ya wataalam wa afya 201 wa fani ya Afisa afya, Afisa tabibu na Fundi sanifu maabara walipata mafunzo juu ya utekelezaji wa mpango huo. Mikoa ambayo mpango huo unatekelezwa hadi sasa imefikia 15 ambapo mikoa mingine ni Dodoma, Singida, Manyara, Kigoma, Rukwa, Katavi, Tabora na Njombe.

### **2.8.2 Uchunguzi wa mlipuko wa ugonjwa uliosababishwa na sumukuvu**

Uchunguzi wa mlipuko wa ugonjwa uliosababishwa na sumukuvu ulifanyika katika Wilaya ya Kondoa na Chemba ambako watu 68 waliripotiwa kuugua na kati yao 20 walipoteza maisha.

Katika uchunguzi huo sampuli 149 za nafaka na karanga zilichukuliwa na kufanyiwa uchunguzi wa sumukuvu aina ya aflatoxin ambapo matokeo yalionesha kuwa sampuli 68 zilikuwa na *aflatoxin* kwa kiwango kisichovumilika. Uchunguzi huo pia ulihuisha sampuli za damu kutoka katika kaya zilizoathirika ambapo kiasi kikubwa cha *aflatoxin* kilikutwa katika sampuli zote. Uwepo wa kiasi kikubwa cha *aflatoxin* katika chakula na damu za waathirika ulithibitisha kuwa madhara ya kiafya na vifo vilivyotokea vilisababishwa na “Acute aflatoxicosis”.

Mamlaka pia ilifanya uchunguzi zaidi katika nafaka na karanga kutoka katika Wilaya 10 ambazo ni Kiteto, Gairo, Mpwapwa, Kongwa, Chamwino, Dodoma Manispaa, Bahi, Singida Vijijiini, Ikungi na Manyoni. Matokeo yalionesha kuwa sampuli 135 kati ya 694 (19%) zilikuwa na uchafuzi wa sumukuvu aina ya aflatoxin kwa kiwango kisichovumilika. Mchanganuo wa sampuli zilizokusanywa pamoja na matokeo ya uchunguzi ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 6

**Jedwali Na. 6: Matokeo ya uchunguzi wa sumukuvu katika nafaka na karanga**

Aina ya Sampuli	Idadi ya sampuli zilizochunguzwa	Zilizofaulu (%)	Zisizokidhi viwango* (%)	Wastani wa uchafuzi kwa sampuli zisizokidhi viwango ( $\mu\text{g}/\text{kg}$ )	Wigo wa uchafuzi kwa sampuli zisizokidhi viwango ( $\mu\text{g}/\text{kg}$ )
Mahindi (unga na nafaka)	485	387 (80)	98 (20)	57.7	5.3 - 298.0
Karanga	87	53 (61)	34 (39)	177.6	10.3 - 340.4
Mtama	76	74 (97)	2 (3)	20.1	7.7 - 31.0
Ulezi	37	36 (97)	1 (3)	40.9	-
Uwele	9	9 (100)	0 (0)	0	-
<b>Jumla</b>	<b>694</b>	<b>559 (81)</b>	<b>135 (19)</b>	<b>80.1</b>	<b>5.3 - 340.4</b>

\* Kiasi cha uchafuzi ni zaidi ya  $5\mu\text{g}/\text{kg}$  kwa *aflatoxin B*<sub>1</sub> pekee au zaidi ya  $10\mu\text{g}/\text{kg}$  kwa aina zote za *aflatoxin (aflatoxin B*<sub>1</sub>, *B*<sub>2</sub>, *G*<sub>1</sub> & *G*<sub>2</sub>)

Hali hii inaonesha kuwa bado iko haja ya kuendelea kuweka kipaumbele katika udhibiti wa vyakula tajwa hususan mahindi na karanga.



Wataalam wa kitaifa na kimataifa wakiwa katika picha ya pamoja na Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wakati wa mukutano wa kuweka mikakati ya udhibiti wa sumukuvu katika bara la Afrika

## 2.9 Ufuatiliaji wa Usalama wa Dawa na Bidhaa Nyongeza

Mfumo mpya wa kielektroniki wa utoaji wa taarifa za madhara ya dawa ulikamilishwa na kuzinduliu rasmi tarehe 12 Oktoba 2016. Katika kipindi hiki, taarifa 271 za madhara yanayohisiwa kusababishwa na matumizi ya dawa zilipokelewa ambapo 94 (34%) kati yake zilipokelewa kuitia mfumo mpya wa kielektroniki. Taarifa zote zilifanyiwa tathmini na kuingizwa kwenye kanzi data (Vigiflow database).

Jumla ya taarifa 103 za usalama wa dawa (Periodic Safety Update Reports - PSUR) zilipokelewa na 38 kati ya hizo zilifanyiwa tathmini. Kufuatia tathmini iliyofanywa, dawa hizo zimeonekana kuwa salama na zinafaa kuendelea kutumika. Sampuli 65 zilizobaki zitatathiminiwa kuanzia robo ya kwanza ya mwaka 2017/18.



Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mhe. Ummey Mwalimu (Mb.) akipata maelezo ya namna ya kutumia simu ya mkononi katika kutoa taarifa inayohusiana na madhara ya dawa

Vilevile, Mamlaka ilihamasisha watendaji 569 wa afya kutoka mikoa ya Dar es salaam, Pwani, Dodoma, Arusha, Morogoro, Lindi, Ruvuma, Kigoma, Tabora, Katavi na Simiyu juu ya utoaji wa taarifa za madhara ya dawa kwa kutumia fomu za njano na kwa mfumo mpya wa kielektroniki.

Mafunzo pia yalitolewa juu ya utoaji wa taarifa za madhara na matukio ya vifaa tiba kwa watoa huduma 664 kutoka vituo vya afya 52 vilivyoko Dar es salaam, Dodoma, Mbeya na Pwani.

## 2.10 Udhibiti wa Majaribio ya Dawa

Majaribio ya dawa 36 yalikaguliwa katika vituo vilivyopo Mikoa ya Mbeya, Kilimanjaro, Mwanza, Dar es Salaam, Tanga na Pwani. Aidha, taarifa 105 za matukio makubwa ya kiafya katika majaribio ya dawa (Serious Adverse Events – SAE) zilipokelewa na kufanyiwa tathmini ambapo hapakuwa na matukio yaliyohusiana na dawa zinazofanyiwa majaribio.

## 2.11 Ufuatiliaji wa Ubora wa bidhaa katika soko

### 2.11.1 Dawa

Mamlaka ilikusanya jumla ya sampuli 467 ambazo zilifanyiwa uchunguzi wa ubora wake ikiwa ni pamoja na tathmini ya taarifa za lebo na karatasi yenye taarifa za dawa (product leaflet). Kati ya sampuli hizo, 337 zilikuwa za dawa za binadamu na 130 dawa za mifugo. Matokeo ya tathmini yalionesha dawa husika kutokidhi matakwa ya lebo. Aidha matokeo ya maabara yalionesha sampuli 3 za dawa za binadamu zenye mchanganyiko wa *diclofenac* na *paracetamol* za vidonge na sampuli 8 za dawa za mifugo aina ya *oxytetracycline 20%* kutokidhi viwango vya ubora. Vilevile sampuli 9 za dawa aina ya *albendazole* hazikukidhi kipimo cha “*dissolution*” kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali Na. 7

**Jedwali Na.7: Mchanganuo wa sampuli zilizokusanywa**

Aina ya dawa		Zilizokusanywa na kufanyiwa Tathmini (PIR)	Uchunguzi wa awali (Screening)	Uchunguzi wa kina (Confirmatory testing)	Zilizofaulu	Zisizokidhi viwango
Dawa za binadamu	Diclofenac /Paracetamol	140	0	139	136	3
	Albendazole	122	122	13	4	9
	Dexamethasone /Neomycin	75	0	71	71	0
	<b>Jumla ndogo 1</b>	<b>337</b>	<b>122</b>	<b>223</b>	<b>211</b>	<b>12</b>
Dawa za Mifugo	Oxytetracycline 10%	58	0	58	58	0
	Oxytetracycline 20%	72	0	72	64	8
	<b>Jumla ndogo 2</b>	<b>130</b>	<b>0</b>	<b>130</b>	<b>122</b>	<b>8</b>
<b>Jumla Kuu (1+2)</b>		<b>467</b>	<b>122</b>	<b>353</b>	<b>333</b>	<b>20</b>

Mamlaka pia iliandaa machapisho ya kisayansi matatu (3) ambapo chapisho la ubora wa dawa za kutibu ugonjwa wa malaria liitwalo *Post Marketing Surveillance of Anti-Malarial Medicines in Tanzania* ilitolewa katika Jarida la Kimataifa la *Pharmaceutical Regulatory Affairs*. Machapisho mengine kuhusu ubora wa dawa za kutibu ugonjwa wa shinikizo la damu pamoja na ubora wa dawa za mifugo yapo katika hatua za mwisho kabla ya kuwasilishwa kwenye majorida ya kimataifa.

Aidha, katika kipindi hiki, Mpango mpya wa ufuatiliaji wa ubora wa dawa katika soko (Post Marketing Surveillance – PMS Programme) kwa miaka mitatu 2017 - 2020 uliandaliwa.

### 2.11.2 Vifaa tiba na Vitendanishi

Jumla ya sampuli 290 za vifaa tiba zilikusanywa kwenye soko katika mikoa ya Dar es salaam, Kigoma, Mwanza, Mtwara na Kilimanjaro. Aina ya sampuli za vifaa tiba zilizokusanywa ni *BP machines* (8), *condoms* (60), *IV canula* (85), *feeding tubes* (29), *cotton wools* (56) na *bandages* (52) ambapo vyote vilifaulu.

### 2.11.3 Chakula

Mpango wa ufuatiliaji katika soko wa bidhaa za chakula zilizosajiliwa (Food Post Marketing Surveillance) ulitekelezwa ambapo jumla ya sampuli 62 za unga wa ngano, 33 za *bread improvers* na 94 za vinywaji baridi visivyokuwa na gesi (*non-carbonated non-alcoholic beverages*) zilichukuliwa na kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara.

Matokeo ya uchunguzi yalionesha kuwa sampuli zote za unga wa ngano zilifaulu vigezo vya usalama vilivyo chunguzwa. Aidha, sampuli 49 (52%) za vinywaji baridi visivyokuwa na gesi zilikutwa na kikolezo aina ya *Saccharine* na sampuli moja (1) ilikutwa na kiwango kisichoruhusiwa cha kikolezo cha *Benzoinic acid* kinachotumika katika uhifadhi wa bidhaa (preservative). Vilevile, lebo za vinywaji husika hazikuonesha kuwa bidhaa hizo zilikuwa na kiambato cha *saccharine*.

Mamlaka pia ilifanya tathmini na ufuatiliaji wa madai mbalimbali yaliyosambazwa kuitia mitandao ya kijamii kuhusu usalama wa bidhaa za chakula aina ya *Banana baby food*, Maji ya kunywa ya “*DEW*”, Soda aina ya Novida, “Chama snacks”, Mafuta ya Alizeti na Mclele wa plastiki kwa lengo la kuthibitisha ukweli wake. Matokeo ya ufuatiliaji yamethibitisha kuwa taarifa hizo zilikuwa za upotoshaji na zimekuwa zikisababisha hofu kwa wananchi. Bidhaa zilizotolewa madai potoshí na hatua zilizochukuliwa zimeoneshwa katika kiambatisho I.

## **2.12 Uteketezaji wa bidhaa zisizokidhi viwango vyta ubora na usalama**

